USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI

TZ21
21ST CENTURY BASIC EDUCATION PROGRAM

SMZ
SERIKALI YA MAPINDUZI ZANZIBAR

# MUONGOZO WA UFUNDISHAJI KUSOMA

# Darasa la 2
# KISWAHILI

21st Century Basic Education Program (TZ21)

# MUONGOZO WA UFUNDISHAJI KUSOMA

# Darasa la 2
# Kiswahili

Januari 2013

*Muongozo huu wa kufundisha usomaji ka darasa la pili umechapishwa na TZ21kwa msaada wa watu wa  Marekani kupitia shirika la msaada la Marekani (USAID) na kuwezeshwa na Creative Associates International. Yaliyomo katika kitini hiki yanatokana na mwandishi na mchapishaji wake na hayawakilishi maoni na msimamo wa USAID wala Serikali ya Marekani.*

# Shukrani

Mpango wa Elimu wa TZ21 unapenda kutoa shukrani za dhati kwa watu wote kwa kutoa msaada wa kiufundi, kitaaluma na kifedha ambao umesaidia katika maendeleo, tafsiri, kuhariri na kuchapisha kitini hiki cha kumfundisha mwalimu. Shukurani za pekee zinaelekezwa kwa WEMA Zanzibar;Taasisi ya Elimu Zanzibar, Taasisi ya Elimu Tanzania, Vyuo vya Ualimu, Dkt Diane Prout na Lynn Evans (), Msimamizi Mkuu wa Programu (Renuka Pillay) kwaajili ya mpango wa Elimu na walimu wa Skuli za Msingi.

Katika hali halisi si rahisi kuutaja kila mchango uliotolewa kufanikisha kazi hii. Walimu wengi wenye moyo wa kujitolea na wataalamu mbalimbali walishiriki katika kazi hii. Tunapenda kuwataja baadhi yao.

| | | |
|---|---|---|
| • | **Maryam Abdullah Yusuf** | Kamishna wa Elimu kutoka WEMA Zanzibar |
| • | **Yahya I A'wakr** | Mkaguzi Mkuu wa Elimu kutoka WEMA Zanzibar |
| • | **Sichana H. Foum** | Mkurugenzi wa Shirika la Huduma za Maktaba kutoka WEMA Zanzibar |
| • | **Uleid Juma Weldi** | Mkurugenzi wa Elimu ya Maandalizi na Msingi kutoka WEMA Zanzibar. |
| • | **Ameir S.H Njeketu** | Mkurugenzi wa Baraza la Mitihani kutoka WEMA Zanzibar) |
| • | **Suleiman Y. Ame** | Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu kutoka WEMA ( Zanzibar) |
| • | **Omar Said Ali** | Mkurugenzi wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kutoka WEMA Zanzibar |
| • | **Charles Nonga** | Msimamizi Msaidizi wa Programu TZ 21 Zanzibar |
| • | **Mohamed Ali Mohamed** | Mkuza Mitaala Mkuu wa Taasisi ya Elimu kutoka WEMA Zanzibar |
| • | **Said S. Al – Abry** | Mkuu wa Divisheni wa Kituo cha Taifa cha Walimu (NTRC) kutoka WEMA Zanzibar |
| • | **Ame J. Khatib** | Afisa wa Elimu ya Msingi kutoka WEMA Zanzibar |
| • | **Hassan Khamis Juma** | Mkuu wa Utayarishaji wa Vitabu kutoka Maktaba Kuu Zanzibar |
| • | **Hamad P. Simai** | Mkuu wa Divisheni ya Usanifu wa Vifaa vya Kufundishia na Kujifunzia |
| • | **Othman Sharif** | Mtaalamu wa Utafiti na Kumbukumbu kutoka TZ 21 Zanzibar |
| • | **Lawrence Kunambi** | Mratibu wa Mitaala wa Taasisi ya Elimu Tanzania kutoka WEMA (Tanzania) |

| | | |
|---|---|---|
| • | **Brandina Milumba** | Mkaguzi wa Skuli kutoka Manispaa ya Mtwara |
| • | **Zahor Mwalim Muhidin** | Mkufunzi kutoka Chuo cha Kiislamu |
| • | **Ali Mwalimu Rashid** | Mtalamu wa lugha kutoka Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar |
| • | **Hamisi Mwaya** | Mkufunzi kutoka chuo cha Ualimu Kitangili |
| • | **Zainabu Ngwende** | Chuo cha Ualimu Mtwara |
| • | **Maulid Lipagati** | Chuo cha Ualimu Mtwara |
| • | **Veronica Macha** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Chang'ombe Dar es Salaam |
| • | **Mary Simumba** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Mbuyuni Dar es Salaam |
| • | **Royce Nyoni** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Mbuyuni Dar es Salaam. |
| • | **Subira Iddi Khamis** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Mkunazini Zanzibar |
| • | **Fatuma Karande** | Mwalimu kutoka Skuli ya Msingi Kibasila Mtwara |
| • | **Aristarick Lyimo** | Mratibu wa Mradi kutoka Mradi wa vitabu vya watoto |
| • | **Justin Machela** | Mpango wa Elimu ya Msingi kutoka TZ21 Mtwara. |
| • | **Joseph Mbasha** | Mratibu wa Mafunzo kutoka ofisi za TZ21 Dar es Salaam. |
| • | **Asha M Mohamed** | Mtalaamu wa Elimu kutokaTZ21 Zanzibar |
| • | **Mashauri Heriel** | kutoka ofisi ya Manunuzi na Afisa Ugavi/TEHAMA kutoka TZ21 Dar es Salaam. |
| • | **Daud Kweba** | Afisa Usimamizi na Tathmini kutoka TZ21 Dar es Salaam. |
| • | **Douglas Bell** | Mkurugenzi kutoka IYF |
| • | **Hassan Libingai** | Mratibu Msaidizi wa Mradi wa Vitabu vya Watoto. |
| • | **Dkt Rest Lasway** | Mshauri wa Sera kutoka TZ21 Dar es Salaam. |
| • | **Andrew Muya** | Mratibu Msaidizi wa Mradi kutoka Mradi wa vitabu vya watoto - Mtwara. |
| • | **Cresencia Ngasoma** | Mwalimu kutoka Manispaa ya Ilala. |
| • | **Saada S Rashid** | Mratibu Kituo cha Walimu Bububu kutoka Zanzibar |
| • | **Adrehem Kayombo** | Mtalaam wa Mitaala ya Elimu kutoka TZ21/IYF Ofisi Dar es salaam. |
| • | **Vincent Katabalo** | Meneja wa Mafunzo ya Walimu TZ 21 Ofisi ya Dar es salaam |

# Yaliyomo


Mawanda na Mtiririko wa Kufundisha Usomaji ........ 1

Namna ya kwafundisha wanafunzi kuandika herufi ........ 1

Hatua Saba Zilizo Katika Muongozo wa Mwalimu ........ 2

Mtiririko wa somo ........ 3

Malengo ya Muongozo ........ 3

1.0 Kufundisha sauti mM na Aa ........ 4

2.0 Kufundisha sauti mM na Aa ........ 7

3.0 Kufundisha sauti kK ........ 12

4.0 Marudio ya sauti mM, Aa na kK ........ 16

5.0 Kufundisha sauti iI ........ 20

6.0 Kufundisha sauti mM na Aa ........ 24

7.0 Kufundisha sauti mM na Aa ........ 28

8.0 Marudio ya sauti ........ 32

9.0 Kufundisha sauti tT ........ 35

10.0 Kufundisha sauti uU ........ 39

11.0 Kufundisha sauti pP ........ 43

12.0 Marudio ya sauti tT, uU na pP ........ 47

13.0 Marudio ya sauti iI, mM na uU ........ 51

14.0 Marudio ya sauti (chagua herufi kutoka siku tofauti) ........ 54

15.0 Marudio ya sauti (chagua herufi kutoka siku tofauti) ........ 58

16.0 Marudio ya sauti (chagua herufi kutoka siku tofauti) ........ 61

17.0 Kufundisha sauti eE ........ 65

18.0 Kufundisha sauti bB ........ 69

19.0 Kufundisha sauti jJ ........ 73

20.0 Marudio ya herufi kubwa na ndogo .......... 77
21.0 Kufundisha herufi fF .......... 81
22.0 Kufundisha herufi dD .......... 84
24.0 Marudio ya herufi kubwa na ndogo .......... 93
25.0 Kufundisha herufi lL .......... 96
26.0 Kufundisha herufi gG .......... 100
27.0 Kufundisha herufi zZ .......... 104
28.0 Marudio ya herufi kubwa na ndogo .......... 108
29.0 Marudio (chagua herufi kutoka siku tofauti).......... 112
30.0 Marudio (chagua herufi kutoka siku tofauti) .......... 115
31.0 Marudio (chagua herufi kutoka siku tofauti) .......... 119
32.0 Marudio (chagua herufi kutoka siku tofauti) .......... 122
33.0 Marudio (chagua herufi kutoka siku tofauti) .......... 126
35.0 Kufundisha herufi rR .......... 134
36.0 Kufundisha herufi hH .......... 138
37.0 Marudio (Herufi kubwa na ndogo).......... 142
38.0 Kufundisha herufi vV .......... 145
39.0 Kufundisha herufi thTH .......... 149
40.0 Kufundisha herufi shSh.......... 153
41.0 Marudio ya herufi kubwa na ndogo .......... .157

# Mawanda na Mtiririko wa Kufundisha Usomaji

Katika muongozo huu istillahi mpya, shughuli za kufanya, na vifupi vya maneno vimefafanuliwa. Hata hivyo baadhi yake zinahitaji ufafanuzi wa ziada ili kueleweka vizuri kwa mwalimu.

## Namna ya kwafundisha wanafunzi kuandika herufi

**Mwalimu**: Shika kadi ya herufi au iandike ubaoni

- **Mwalimu: Fuatisha umbo la herufi na kisha useme**:
- ***Nitazame: Tazama maandishi***
- **Chunguza herufi** – Mwalimu aoneshe uandishi wa herufi. (Unapoandika herufi upana wake unatakiwa ulingane na upana wa mkono wako. Nafasi kati ya herufi na herufi lazima iwe unene wa kidole cha kati na shahada vilivyoungana
- Mwalimu anasema:**[sauti ya herufi]]**
- Angalia ninayoandika**[sauti ya herufi]**
- ***[Hatua ya 1, 2, 3, nk. ya kuandika herufi].***
- ***Rudia sauti ya herufi kila unapofuatisha umbo la herufi***
- **Mwalimu**: Shika kadi ya herufi au iandike ubaoni
- **Mwalimu: Fuatisha umbo la herufi na kisha useme**:
- ***Nitazame: Tazama maandishi***
- **Chunguza herufi** – Mwalimu aoneshe uandishi wa herufi. (Unapoandika herufi upana wake unatakiwa ulingane na upana wa mkono wako. Nafasi kati ya herufi na herufi lazima iwe unene wa kidole cha kati na shahada vilivyoungana
- Mwalimu anasema:**[sauti ya herufi]]**
- Angalia ninayoandika**[sauti ya herufi]**
- ***[Hatua ya 1, 2, 3, nk. ya kuandika herufi].***
- ***Rudia sauti ya herufi kila unapofuatisha umbo la herufi***

**Mfano:**

- Niangalie. Tazama maandishi.
- /b/

**Chunguza umbo**

- Anzia juu
- Chora mstari kushuka chini
- Chora duara

**Mfano:**

- Niangalie. Tazama maandishi.
- /b/

**Chunguza umbo**

- Anzia juu
- Chora mstari kushuka chini
- Chora duara
- Maneno yaliyokolezwa na kulalia upande huashiria maneno ya mwalimu.
- Maneno yaliyo katika mabano – kwa mfano: (wakati wa kuonesha kila herufi) – Hueleza matendo ya mwalimu wakati anapotamka maneno yaliyokolezwa na kulalia upande.
- Maneno yaliyokolezwa na kulalia upande yakiwa katika mabano au vitenganishi ni - ***/Sauti ya herufi/***, ***[neno]***, ***[Jina la mwanafunzi],*** etc. – Hufafanua maneno yanayotamkwa na mwalimu.
- Maneno yaliyo kawaida katika mabano– [neno], [sauti ya herufi], n.k Huelezea maneno yanayotamkwa na mwanafunzi
- inamaanisha "ndiyo"
- inamaanisha "hapana"
- imaanisha "toa msaada"
- Inamaanisha mwalimu aseme "sikiliza"

## Hatua Saba Zilizo Katika Muongozo wa Mwalimu

1. Mapitio ya herufi ★
   a. **Somo lililopita**
      Sauti
      Umbo
   b. Mchanganyiko – Sauti tatu zilizofundishwa mara ya mwisho katika utaratibu uliochanganywa
2. Utambuzi wa Sauti ★
   a. **Maneno mchanganyiko** – kutoka kwenye masomo yaliyotangulia
   b. **Herufi mpya iliyo katika neno** – sauti ya herufi mpya ya mwanzo
3. **Herufi mpya** ★
   a. **sauti**
   b. **Umbo**
4. **Unganisha na kutenganisha silabi**★
   a. **Herufi mpya** – Unganisha silabi na herufi mpya
   b. **Machanganyiko** – Unganisha mchanganyiko wa silabi mbili
5. **Unganisha na tenganisha maneno**★
   a. **Mchanganyiko wa maneno-**
6. **Andika**★
   a. **Herufi Mpya** –
   b. **Herufi tatu zilizofundishwa kabla** –
7. **Andika SENTENSI, hadithi au wimbo**

## Mtiririko wa somo

## Malengo ya Muongozo

Muongozo huu si mbadala wa andalio la somo, bali humwongoza mwalimu kikamilifu na kimantiki katika kufanya yafuatayo:

- Kufundisha usomaji kwa kuzingatia shughuli ya mwalimu, shughuli ya mwalimu na mwanafunzi na shughuli ya mwanafunzi peke yake katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

- Kuimarisha ufundishaji wa usomaji kwa kumwongoza mwalimu namna ya kuwafundisha wanafunzi wa darasa la II uhusiano wa sauti na herufi na matumizi yake katika kuunda na kusoma maneno.

- Kuwashirikisha wanafunzi katika usomaji kwa kuwapa shughuli mbalimbali zitakazowawezesha kujenga ujuzi katika stadi ya kusoma wakati wa kujifunza.

Kufundisha usomaji kwa darasa la pili kunazingatia zaidi maneno yenye kuundwa na silabi tatu tofauti na darasa la kwanza ambao huzingatia maneno yenye kuundwa na silabi mbili.

Kutakuwa na marudio ya wiki, ambayo yatafanyika kila siku za ijumaa; na pia marudio ya mwezi ambayo yatafanyika wiki ya nne katika kila mwezi.

Kwa hiyo ni muhimu kwa mwalimu kujua kuwa, muongozo huu utatumika sanjari na muhtasari wa somo, vitabu vya kiada na ziada pamoja na rejea mbalimbali kwa ajili ya kujenga umahiri katika stadi ya kusoma. Aidha, Mwalimu atatumia maudhui ya muongozo huu katika kufundisha usomaji kwa kuzingatia mazingira ya darasa lake kwa mfano, ukubwa wa darasa, idadi na umri wa wanafunzi.

*Weka alama ya **(√)** baada ya kufundisha*

## 1.0 Kufundisha sauti mM na Aa
## Wiki ya 1: Siku ya 1

| | |
|---|---|
| Tarehe: ____________________<br>Muongozo wa ufundishaji: Tumia jina la herufi/sauti ya herufi katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika<br><br>Malengo:<br>• Kufundisha sauti na jina la herufi mM, aA kwa kutumia muongozo ufuatao<br>• Mwanafunzi aweze Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi<br>• Mwanafunzi aweze Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi | Zana:<br>• Kadi za herufi mM, aA<br>• Kadi za herufi kwa ajili ya marudio<br>• Kadi za maneno<br>• Andika neno [mama] ubaoni<br>• Kadi za sentensi<br>• Hadithi au Wimbo<br>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi |

## Muongozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 5)

Fundisha sauti ***mM, aA*** kwa kutumia muongozo ufuatao:

| **Ujuzi** | **Mwalimu "Ninatenda"** | **Mwalimu na mwanafunzi "tunatenda" Rudia sauti zote na maneno** | **Mazoezi ya mwanafuzi "unatenda"** |
|---|---|---|---|
| Utambuzi wa Sauti<br><br>(USIANDIKE) | Sauti mwanzo ya neno [mama] ni? /m/ Sikiliza, /mmmm/<br><br>Sasa, sauti ya mwanzo ya neno [ama] ni? /a/ Sikiliza, /aaaa/<br><br>Sauti mwanzo ya neno [mate] ni? /m/ Sikiliza, /mmm/<br><br>Sasa, sauti ya mwanzo ya neno [amani] ni? /a/ Sikiliza, /aaaa/ | Sasa, tuseme sauti ya mwanzo neno [mama] Kilammoja, sauti ya mwanzo ya neno [mama] ni /mmmm/<br><br>Mwalimu awaongoze wanafunzi kutamka sauti kwa kunyanyua mkono na kushusha akisema. (Haya sote tuseme) /mmmm/<br><br>Sasa, fundisha sauti ya mwanzo ya neno [mate] kama ulivyofanya kwa [mama]<br><br>Sasa, tuseme sauti ya mwanzo neno [ama] Kilammoja, sauti ya mwanzo ya neno [ama] ni /aaaa/<br><br>Mwalimu awaongoze wanafunzi kutamka sauti kwa kunyanyua mkono na kushusha akisema. (Haya sote tuseme) /aaaa/<br><br>Sasa, fundisha sauti ya mwanzo /a/ ya neno [amani] kama ulivyofanya kwa [ama] | Mwalimu aulize: Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia? (Rejea maneno ya masomo yaliyopita)<br>• Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?<br>Wanafunzi watasema:<br>• Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?<br>Wanafunzi watasema:<br>• Wasichana wote, sauti ipi?<br>Wanafunzi watasema:<br>• Wavulana wote, sauti ipi?<br>Wanafunzi watasema:<br>• Upande wangu wa kulia, sauti ipi? (mwalimu elekeza mkono upande wa kulia)<br>Wanafunzi watasema:<br>• Upande wangu wa kushoto, sauti ipi? (mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto)<br>Wanafunzi watasema:<br>• Wote pamoja, sauti ipi?<br>Wanafunzi watasema: |

## Mazoezi ya utambuzi wa sauti

**Mchezo wa sauti:**

- Waambie wanafunzi wasimame wanaposikia sauti ya mwanzo ya maneno waliyojifunza (USIYAANDIKE) ) [***amani, mama, asante, maji, mawe, saa, ana, ama]***
- Sahihisha makosa

## Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (Dakika 3-4)

**Marudio:**

- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie: **TAZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi za herufi ***mM*** kisha waulize hizo ni herufi gani
- Fanya hivyo kwa herufi ***aA***
- Uliza wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja anafahamu majina ya herufi.

Fundisha majina ya herufi ***mM, aA*** kutumia muongozo ufuatao

| | | | |
|---|---|---|---|
| Msingi wa kialfabeti<br><br>Uhusiano wa Sauti na herufi<br><br>(ANDIKA) | Mwalimu: "Ninatenda" TAZAMA MAANDISHI.<br><br>Hii ni herufi m. Onesha wanafunzi herufi mM. Herufi mM inaunda sauti /mmmm/.<br><br>Hii ni herufi aA Onesha wanafunzi aA. Herufi a inaunda sauti /aaaa/. | Mwalimu na mwanafunzi: "Tunatenda"<br><br>TAZAMA MAANDISHI.<br>Sasa, kila mmoja: Hii ni herufi mM. (Onesha wanafunzi herufi mM) Herufi mM inaunda sauti gani, sote kwa pamoja?<br>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) /mmmm/<br><br>Sasa, kilammoja: Hii ni herufi aA. (Onesha wanafunzi herufi aA). Herufi aA inaunda sauti gani, sote kwa pamoja?<br>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) /aaaa/ | mwanafunzi: "Unatenda"<br><br>Mwalimu wagawie wanafunzi kadi za herufi katika makundi na waambie wachague herufi zinazoendana na sauti zilizotamkw |

★ **Mazoezi ya sauti ya herufi na ufasaha (4-5 dakika): MAZOEZI**

- Chukua kadi zenye herufi: ***mM, aA*** (AU andika herufi hizo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi kisha onesha moja baada ya nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.

**(Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii)**

- Tamka sauti ya herufi ***mM***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo. Fanya hivyo kwa herufi ***aA***.
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno; ***[mama ama, mate, amani]*** ubaoni kisha sema "**Tazama maandishi**".
- Waoneshe namna ya kutamka sauti za herufi (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**). ***/m/ /a/ / m/ /a/,***
- Unganisha sauti kisha sema neno **[mama].**
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno ***[ama]*** kisha watamke neno lote.
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno.
- Onesha neno kasha waambie wanafunzi walitamke (**Mnatenda**).
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno ***[mama]*** ni ***/mmmm/,*** inayofuata ***/aaaa/,*** inayofuata ***/mmmm/,*** ya mwisho ***/aaaa/.*** Neno gani hilo? ***[mama].*** Neno hilo ni ***[mama].***
- Sasa zamu yenu. Ni neno gani? ***[mama]***
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hiki. **(Ninatenda, Tunatenda, Unatenda)**

**Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno; ***[amani, mama, mama, asante, maji, mawe, ana, ama]***

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

## Msamiati: (Dakika 4-5)

RUDIA MANENO; ***[amani, mama, mama, asante, maji, mawe, ana, ama]***

## Ufahamu wa kusikiliza (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea amekozeshwa na yamepigiwa mstari. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kusoma hadithi, tulia kwa muda kisha onesha msamiati huo ubaoni.

## Ufahamu

**Rejea ya neno la akiba:**

- Andika neno ***[mama]*** ubaoni.

- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa. Waeleze walitumie katika sentensi kwa usahihi.

*Weka alama ya* **(√)** *baada ya kufundisha*

## 2.0 Kufundisha sauti mM na Aa
## Wiki ya 1: Siku ya 2

| | |
|---|---|
| Tarehe: ____________________<br>Muongozo wa ufundishaji: Tumia jina la herufi/sauti ya herufi katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika<br>Malengo:<br>• Kufundisha sauti na jina la herufi mM, aA kwa kutumia muongozo ufuatao<br>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma hadithi | Zana:<br>• Kadi za herufi mM, aA<br>• Kadi za herufi kwa ajili ya marudio<br>• Kadi za maneno<br>• Andika neno [Mama, Ama] ubaoni<br>• Kadi za sentensi<br>• Hadithi au Wimbo<br>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi |

## Muongozo wa kufundisha **utambuzi wa sauti (Dakika 5)**

## Marudio:

- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo: ***/m/, /a***/
- Uliza wanafunzi sauti ipi wanayosikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita (**Usiandike Maneno**). ***[mama, ama, amani]***
- Uliza wanafunzi sauti za mwanzo ***/m/, /a/***

Fundisha sauti ***mM, aA*** kwa kutumia muongozo ufuatao:

| **Ujuzi** | **Mwalimu "Ninatenda"** | **Mwalimu na Mwanafunzi "tunatenda" Rudia sauti zote na maneno** | **Mazoezi ya mwanafunzi "unatenda"** |
|---|---|---|---|
| Utambuzi wa Sauti<br><br>(USIANDIKE) | Sauti mwanzo ya neno [mama] ni? /m/ Sikiliza, /mmmm/<br><br>Sasa, sauti ya mwanzo ya neno [ama] ni? /a/ Sikiliza, /aaaa/<br><br>Sauti mwanzo ya neno [mate] ni? /m/ Sikiliza, /mmm/<br><br>Sasa, sauti ya mwanzo ya neno [amani] ni? /a/ Sikiliza, /aaaa/ | Sasa, tuseme sauti ya mwanzo neno [mama]<br>Kila mmoja, sauti ya mwanzo ya neno [mama] ni /mmmm/<br>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe (Haya sote tuseme) /mmmm/<br><br>Sasa, tuseme sauti ya mwanzo ya neno [ama] Kilammoja, sauti ya mwanzo ya neno [ama] ni /aaaa/ Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (Haya sote tuseme) /aaaa/<br><br>Sasa, fundisha sauti za mwanzo za maneno [mate, amani] kama ulivyofanya kwa [mama] na [ama] | Mwalimu aulize: Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia?<br>• Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi? Wanafunzi watasema:<br>• Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi? Wanafunzi watasema:<br>• Wasichana wote, sauti ipi? Wanafunzi watasema:<br>• Wavulana wote, sauti ipi? Wanafunzi watasema:<br>• Upande wangu wa kulia, sauti ipi? (mwalimu elekeza mkono upande wa kulia) Wanafunzi watasema:<br>• Upande wangu wa kushoto, sauti ipi? (mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto) Wanafunzi watasema:<br>• Wote pamoja, sauti ipi? Wanafunzi watasema: |

## Mazoezi ya utambuzi wa sauti

**Mchezo wa sauti:**

- Wambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao juu ya dawati wakati wa mchezo huu wa sauti.
- Wambie wanafunzi waoneshe dole gumba juu wanaposikia sauti ***/m/*** na dole gumba chini wasipoisikia sauti hiyo mwanzoni mwa maneno yafuatayo: (USIYAANDIKE) [***amani, mama, asante, maji, mawe, saa, ana, ama]***

  Maana yake "Ndiyo" Maana yake "hapana"
- Ita mwanafunzi mmoja mmoja aseme neno linaloanza na sauti ***/m/.***
- Sahihisha makosa

**Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (**Dakika 3-4**)**
**Marudio:**

- Rudia herufi ulizofundisha: ***m, a***
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie: **TAZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi ***m*** kisha waulize hiyo ni herufi gani
- Fanya hivyo kwa herufi ***a***
- Uliza wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja anafahamu majina ya herufi.

Fundisha majina ya herufi ***mM, aA*** kutumia muongozo ufuatao.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Msingi wa kialfabeti<br><br>Uhusiano wa Sauti na herufi<br><br>(ANDIKA) | Mwalimu: "Ninatenda"<br>TAZAMA MAANDISHI.<br><br>Hii ni herufi mM. Onesha wanafunzi herufi mM. Herufi mM inaunda sauti /mmmm/.<br><br>Onesha wanafunzi aA. Herufi aA inaunda sauti /aaaa/. | Mwalimu na mwanafunzi: "Tunatenda"<br><br>TAZAMA MAANDISHI.<br>Sasa, kila mmoja: Hii ni herufi mM. (Onesha wanafunzi herufi mM) Herufi mM inaunda sauti gani, sote kwa pamoja?<br>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) /mmmm/<br><br>Sasa, kilammoja: Hii ni herufi aA. (Onesha wanafunzi herufi aA). Herufi a inaunda sauti gani, sote kwa pamoja? Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) /aaaa/ | Mwanafunzi: "Unatenda"<br>Sasa zamu yenu. Darasa hii ni herufi? (Onesha herufi mM, aA)<br>• Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?<br>Wanafunzi watasema:<br>• Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?<br>Wanafunzi watasema:<br>• Wasichana wote, sauti ipi? Wanafunzi watasema:<br>• Wavulana wote, sauti ipi?<br>Wanafunzi watasema:<br>• Upande wangu wa kulia, sauti ipi? (mwalimu elekeza mkono upande wa kulia)<br>Wanafunzi watasema:<br>• Upande wangu wa kushoto, sauti ipi? (mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto)<br>Wanafunzi watasema:<br>• Wote pamoja, sauti ipi?<br>Wanafunzi watasema: |

★**Mazoezi ya sauti ya herufi na ufasaha (4-5 dakika): MAZOEZI**

- Chukua kadi zenye herufi: ***m, M, a, A*** (AU andika herufi hizo ubaoni).

- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi kisha onesha moja baada ya nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.
  **(Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii)**
- Tamka sauti ya herufi ***aA***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo.
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno; ***[Ama]*** ubaoni kisha sema "**Tazama maandishi**".
- Waoneshe namna ya kutamka (**Ninatenda, Tunatenda, Mnatenda**). ***/a/ /m/ /a/.***
- Unganisha sauti kisha sema neno **[Ama]**
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno ***[ama],*** kisha watamke neno lote
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke. (**Mnatenda**).
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno ***[ama]*** ni ***/aaaa/,*** inayofuata ***/mmmm/,*** ya mwisho ***/aaaa/.*** Neno gani hilo? ***[ama].*** Neno hilo ni ***[mama].***
- Sasa zamu yenu. Ni neno gani? ***[ama]***
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hiki. **(Ninatenda, Tunatenda, Unatenda)**

**Sentensi rahisi:**

- Mtoto wa dada ni mrefu sana.
- Kaka ametega mtego wa panya.
- Amani ni mvulana wa darasa la pili
- Watoto wa Mwalimu Abasi wana heshima

**Mazoezi ya Kusoma Sentensi.**

- Waoneshe wanafunzi kila herufi za sauti na utamke **[Mtoto wa dada ni mrefu sana].**
- Waambie wanafunzi wasome sentensi **kwa sauti**
- **Fanya hivyo kwa sentensi zilizosalia.**

## Msamiati: (Dakika 4-5)

RUDIA MANENO; ***[Amani, Mama, Ama, Mate]***

**Rejea neno la akiba:**

- Andika neno **[mama]** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa. Waambie walitumie katika sentensi kwa usahihi

**Neno jipya [*wa]***:

- Waambie wanafunzi kuwa neno jipya lililotumiwa sana ni ***wa***
- Waoneshe kadi ya neno au liandike ubaoni.
- Waambie wanafunzi wasome neno pamoja na wewe.

**Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno; ***[Amani, Mama, Mate, wa]***

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka ,kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

## **Ufahamu wa kusikiliza** (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea yamekolezwa na yamepigiwa mstari.Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kusoma hadithi, tulia kwa muda kisha onesha msamiati huo ubaoni.

## Ufahamu

Hapo zamani, kulikuwa na kijiji kimoja ambacho kilikuwa na misitu na mito mingi. Watu huenda kukusanya kuni na kuchota maji. Siku moja Safia na wenzake walikwenda kukusanya kuni za kupikia. Wakati Safia akikusanya kuni ghafla alimuona mjusi mkubwa akimsogelea. Safia alishtuka na kutupa kuni chini nakuanza kwenda mbio. Mjusi alimuandama Safia kwa mbio, lakini Safia aliweza kumzidi mjusi. Kwa hivyo mjusi alishindwa kumpata.

**Maswali ya Ufahamu:**

- Watu walikwenda kufanya nini katika misitu ya kijiji?
- Je, ni kwa nini Safia alishtuka na kutupa kuni chini?
- Taja majina ya wanyama wanaopatikana msituni?

**Mazoezi**:Waambie wanafunzi watafute maneno yanayoanza na sauti **/m/, /a/**

*Weka alama ya **(√)** baada ya kufundisha*

## 3.0 Kufundisha sauti kK
## Wiki ya 1: Siku ya 4

| | |
|---|---|
| Tarehe: ___________________________<br>Muongozo wa ufundishaji: Tumia jina la herufi/sauti ya herufi katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika<br>Malengo:<br>• Kufundisha sauti na jina la herufi kK kwa kutumia muongozo ufuatao<br>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma hadithi | Zana:<br>• Kadi za herufi kK<br>• Kadi za herufi kwa ajili ya marudio<br>• Kadi za maneno<br>• Andika neno [kitabu] ubaoni<br>• Kadi za sentensi<br>• Hadithi au Wimbo<br>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi |

**Muongozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 5)**

**Marudio**:

- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo: ***/m/,/a/***
- Uliza wanafunzi sauti ipi wanayosikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita (**Usiandike Maneno**). ***[mama, maji, awali, amani]***

Fundisha sauti ***kK*** kwa kutumia muongozo ufuatao:

| Ujuzi | Mwalimu "Ninatenda" | Mwalimu na Mwanafunzi "tunatenda" Rudia sauti zote na maneno | Mazoezi ya mwanafunzi "unatenda" |
|---|---|---|---|
| Utambuzi wa Sauti<br><br>(USIANDIKE) | Sauti mwanzo ya neno [kitabu] ni? /k/ Sikiliza, /k/<br><br>Sasa, sauti ya mwanzo ya neno [kabati] ni? /k/ Sikiliza, /k/ | Sasa, tuseme sauti ya mwanzo neno [kitabu] Kilammoja, sauti ya mwanzo ya neno [kitabu] ni /k/ Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe (Haya sote tuseme) /k/<br><br>Sasa, fundisha sauti za mwanzo za neno [kabati] kama ulivyofanya kwa [kitabu] | Mwalimu aulize: Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia?<br>• Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi? Wanafunzi watasema:<br>• Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi? Wanafunzi watasema:<br>• Wasichana wote, sauti ipi? Wanafunzi watasema:<br>• Wavulana wote, sauti ipi? Wanafunzi watasema:<br>• Upande wangu wa kulia, sauti ipi? (mwalimu elekeza mkono upande wa kulia) Wanafunzi watasema:<br>• Upande wangu wa kushoto, sauti ipi? (mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto) Wanafunzi watasema:<br>• Wote pamoja, sauti ipi? Wanafunzi watasema: |

## Mazoezi ya utambuzi wa sauti

**Mchezo wa sauti:**

- Wambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao juu ya dawati wakati wa mchezo huu wa sauti.
- Wambie wanafunzi waoneshe dole gumba juu wanaposikia sauti ***/k/*** na dole gumba chini wasipoisikia sauti hiyo mwanzoni mwa maneno yafuatayo: (USIYAANDIKE) [***kitabu, amani, nanasi kabati, kijiko, amina, kalamu, koroga, kahawa]***

  Maana yake "Ndiyo"  Maana yake "hapana"
- Ita mwanafunzi mmoja mmoja aseme neno linaloanza na sauti ***/k/.***
- Sahihisha makosa

**Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (**Dakika 3-4**)**
**Marudio:**

- Rudia herufi ulizofundisha: ***m, a***
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie: **TAZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi ***m*** kisha waulize hiyo ni herufi gani
- Fanya hivyo kwa herufi ***a***
- Uliza wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja anafahamu majina ya herufi.

Fundisha majina ya herufi ***kK*** kutumia muongozo ufuatao

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Msingi wa kialfabeti**<br><br>**Uhusiano wa Sauti na herufi**<br><br>**(ANDIKA)** | **Mwalimu: "Ninatenda" TAZAMA MAANDISHI.**<br><br>*Hii ni herufi* ***kK***. Onesha wanafunzi herufi ***kK***. *Herufi* ***kK*** *inaunda sauti* ***/k/.*** | **Mwalimu na mwanafunzi: "Tunatenda"**<br><br>**TAZAMA MAANDISHI.**<br>*Sasa, kila mmoja: Hii ni herufi* ***kK***. (Onesha wanafunzi herufi ***kK***) Herufi ***kK*** *inaunda sauti gani, sote kwa pamoja?*<br>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) ***/k/*** | **Mwalimu:**<br>*Sasa zamu yenu. Darasa hii ni herufi?* (Onesha herufi ***kK***)<br>• ***Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wasichana wote, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wavulana wote, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Upande wangu wa kulia, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kulia)* *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto)* *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wote pamoja, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:* |

★ **Mazoezi ya sauti ya herufi na ufasaha (4-5 dakika):**
**MAZOEZI**

- Chukua kadi zenye herufi: ***Aa, mM, kK*** (AU andika herufi hizo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi kisha onesha moja baada ya nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.

**(Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii)**

- Tamka sauti ya herufi ***kK***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo.
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno ***[kitabu]*** ubaoni kisha sema "**Tazama maandishi**".
- Waoneshe namna ya kutamka (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**). ***/k/ /i/ /t/ /a/ /b/ /u/***
- Unganisha sauti kisha sema neno ***[kitabu].***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno ***[kitabu],*** kisha watamke neno lote
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka maneno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke. (**Mnatenda**).
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno ***[kitabu]*** ni ***/k/,*** inayofuata ***/iiii/,*** inayofuata ***/t/,*** inayofuata ***/aaaa/,*** *inayofuata* ***/b/,*** *ya mwisho* ***/uuuu/.*** Neno gani hilo? ***[kitabu].*** Neno hilo ni ***[kitabu].***
- Sasa zamu yenu. Ni neno gani? ***[kitabu]***
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hiki. **(Ninatenda, Tunatenda, Unatenda)**

**Sentensi rahisi:**

- Baba amenunua kitabu cha kusoma
- Kabati letu ni zuri.
- Kaka ameleta matunda mengi.
- Kijiko cha Rukia ni kidogo.

**Mazoezi ya Kusoma Sentensi**

- Waoneshe wanafunzi kila herufi za sauti na utamke **[Kabati letu ni zuri].**
- Waambie wanafunzi wasome sentensi **kwa sauti**
- **Fanya hivyo kwa sentensi zilizosalia.**

## Msamiati: (Dakika 4-5)

RUDIA MANENO; ***[kitabu, kabati, kijiko, kalamu, koroga, kahawa]***

**Rejea neno la akiba:**

- Andika neno ***[kitabu]*** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa. Waambie walitumie katika sentensi kwa usahihi

**Neno jipya *[ni]*:**

- Waambie wanafunzi kuwa neno jipya lililotumiwa sana ni ***ni***
- Waoneshe kadi ya neno au liandike ubaoni.
- Waambie wanafunzi wasome neno pamoja na wewe.

**Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno; ***[kitabu, kabati, kijiko, kalamu, koroga, kahawa, ni]***

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka , kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

## **Ufahamu wa kusikiliza** (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea yamekolezwa na yamepigiwa mstari.Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kusoma hadithi, tulia kwa muda na onesha msamiati ubaoni.

## Ufahamu.

Baraka na Safia wamepewa kabati zuri la mbao na mama yao. Mama yao aliwataka waweke nguo zao kabatini ili zisipate vumbi. Pia aliwaambia kuwa, wasipoziweka kabatini paka wao Bingo atazichafua na kuzichana.

**Maswali ya Ufahamu:**

- Baraka na Safia wamepewa nini?
- Kwa nini Baraka na Safia wanaweka nguo kabatini?
- Ni vitu gani vingine huwekwa kabatini?
- Je, kuna aina ngapi za kabati

  **Mazoezi**: Waambie wanafunzi watafute maneno yanayoanza na sauti ***/k/***

*Weka alama (√) baada ya kufundisha*

## 4.0 Marudio ya sauti mM, Aa na kK
## Wiki ya 1: Siku ya 5

| | |
|---|---|
| Tarehe: ______________________<br>**Muongozo wa ufundishaji:** Tumia **jina la herufi*/sauti ya herufi*** katika muongozo huu ili kufundisha herufi na sauti za herufi husika<br>**Malengo:**<br>• Mwanafunzi aweze kurudia sauti ya herufi na jina la ***mM, aA, kk*** Kutumia maelekezo ya hapo chini<br>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi kwa kutumia kadi za herufi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi zilizo rahisi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma hadithi | **Zana:**<br>• Kadi za herufi ***mM, aA, kK***<br>• Kadi za herufi kwa ajili ya marudio<br>• Kadi za maneno<br>• Andika neno ***[kabati]*** ubaoni<br>• Kadi za sentensi<br>• Hadithi au Wimbo<br>• Kitini cha mazoezi kwa wanafunzi |

## Muongozo wa kufundisha Utambuzi wa Sauti (Dakika 5)

★ **Marudio**:

- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo: ***/m/, /a/, /k/***
- Uliza wanafunzi sauti ipi wanayosikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita (**Usiandike Maneno)**.

Rudia sauti kwa kutumia muongozo ufuatao.

| **Ujuzi** | **Mwalimu "Ninatenda"** | **Mwalimu na mwanafunzi "Tunatenda"** *Rudia sauti zote za maneno* | **Mazoezi ya mwanafunzi "Unatenda"** |
|---|---|---|---|
| **Utambuzi wa Sauti**<br><br>**(USIANDIKE)** | *Mwalimu aongoze kutambua sauti za mwanzo za maneno tofauti kutoka masomo yaliyotangulia.* | *Sasa, Tuseme sauti ya mwanzo kutoka katika maneno tofauti tuliyojifunza somo lililopita.* | **Mwalimu anasema:** Ni sauti ipi ya mwanzo mnayosikia (Rejea maneno ya masomo yaliyopita)<br>• ***Mistari mitatu ya nyuma, ni sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Mistari mitatu ya mbele, ni sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Wasichana wote, ni sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Wavulana wote, ni sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kulia, sauti ipi?*** *(Mwalimu elekeza mkono upande wa kulia)* *Wanafunzi watasema*<br>• ***Upande wangu, wa kushoto sauti ipi?*** *(Mwalimu aelekeze mkono wa kushoto)* Wanafunzi watasema:<br>• ***Wote pamoja, sauti ipi?*** Wanafunzi watasema: |

## Mazoezi ya Utambuzi wa Sauti

**Mchezo wa Sauti:**

- Waambie wanafunzi wasimame wanaposikia sauti ya mwanzo ya maneno waliyojifunza (USIYAANDIKE)
- Sahihisha makosa

## Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (Dakika 3-4)

**Marudio:**

- Rudia herufi ulizofundishwa ambazo ni ***mM, aA, kK,***
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie: **TAZAMA MAANDISHI.**
- Uliza wanafunzi ni herufi gani na waioneshe ***mM, aA, kK***
- Uliza wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja anafahamu majina ya herufi.
- Chagua herufi kutoka katika masomo yaliyopita ili wanafunzi wayafanyie mazoezi

Rudia majina ya herufi ***mM, aA, kK*** kutumia muongozo ufuatao

| **Msingi wa kialfabeti**<br><br>**Uhusiano wa Sauti na herufi**<br><br>**(ANDIKA)** | **Mwalimu: "Ninatenda"**<br><br>**TAZAMA MAANDISHI.**<br>*Hii ni herufi **mM**.* Onesha wanafunzi ***mM**. Herufi **mM** inatoa sauti **/mmmm/.***<br><br>*Hii ni herufi **aA.*** (Onesha wanafunzi ***a**A.)Herufi **aA** inatoa sauti **/aaaa/.***<br><br>*Hii ni herufi **kK*** (Onesha wanafunzi ***kK***). *Herufi **kK** inatoa sauti **/k/.*** | **Mwalimu na mwanafunzi: "Tunatenda"**<br><br>**TAZAMA MAANDISHI.**<br>*Kila mmoja: Hii ni sauti **mM**.* (Onesha wanafunzi ***mM***.) *Sauti **mM** inatoa sauti gani,kila mmoja?*<br>Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (darasa zima)<br>***/m/***<br><br>Sasa Kila mmoja: Hii ni herufi ***aA***. (Onesha wanafunzi herufi ***aA***.) Herufi ***aA*** inaunda sauti gani, kila mmoja?<br>Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (Darasa zima)<br>***/aaaa/***<br><br>*Sasa, kila mmoja: hii ni herufi .* (Onesha wanafunzi **kK**.) *Herufi **kK** inaunda sauti gani?*<br>Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (darasa zima)<br>***/k/*** | **Mwanafunzi: "Unatenda"**<br><br>Mwalimu wagawie wanafunzi kadi za maneno katika makundi na waambie wachague herufi zinaashiria sauti zilizotamkwa |
|---|---|---|---|

★ **Mazoezi ya Sauti ya herufi na Ufasaha (Dakika 4-5): MAZOEZI**

- Chukua kadi zenye herufi ***mM, aA, kK*** (AU andika herufi hizo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi kisha onesha moja baada ya nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.
  **(Tumia sekunde 30 au zinazokaribiana kwa zoezi hili)**
- Tamka sauti ya herufi ***mM***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema jina la herufi linalounda sauti hiyo. Fanya hivyo kwa **aA, kK.**
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno; ***[mafuta, azima, kabati]*** kwenye ubao na useme **"Tazama Maandishi".**
- Waoneshe namna ya kutamka (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**) ***/m/ /a/ /f/ /u/ /t/ /a/***
- Unganisha sauti kisha sema neno ***[mafuta].*** Fanya hivyo kwa neno ***[azima, kabati].***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizomo katika neno ***[mafuta],*** na kisha watamke neno lote.
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hiyo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke. ***[Mnatenda].***
- Onesha kila herufi kasha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno ***[mafuta]*** ni **/mmmm/**, inayofuata **/aaaa/** inayofuata **/f/**, inayofuata ***/uuuu/***, inayofuata ***/t/,*** ya mwisho **/aaaa/**. Ni neno gani hilo? ***[mafuta].*** Neno ni *[**mafuta**]*.
- Sasa zamu yenu. Neno gani? ***[mafuta]***
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hicho **(Ninatenda, Tunatenda, Unatenda)**

**Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno **[mafuta, matuta, azima akili, kabati, kokota]**

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanpoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonyesha (au onesha maneno hayo ubaoni).
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

## Msamiati: (Dakika 4-5)

Rudia maneno ***[mafuta, matuta, azima, akili, kabati, kokota]***

## Ufahamu wa Kusikiliza (Dakika 10):

Wasomee wanafunzi hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno yamekozeshwa na yamepigiwa mstari. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kusoma hadithi, tulia kwa muda na onesha msamiati huo ubaoni.

## Hadithi ya Kusoma kwa Sauti [Jina la Hadithi]

- Andika jina la hadithi ubaoni.
- Andika jina la mwandishi wa hadithi ubaoni
- Andika jina la msanifu wa michoro ubaoni.

**Rejea neno la akiba:**

- Andika neno ***[mafuta]*** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa. Waambie walitumie katika sentensi kwa usahihi

*Weka alama ya* **(√)** *baada ya kufundisha*

## 5.0 Kufundisha sauti iI
## Wiki ya 2: Siku ya 1

| | |
|---|---|
| Tarehe: ______________________<br>**Muongozo wa ufundishaji:** Tumia **jina la herufi/sauti ya herufi** katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika<br>**Malengo:**<br>• Kufundisha sauti na jina la herufi ***iI*** kwa kutumia muongozo ufuatao<br>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma hadithi | **Zana:**<br>• Kadi za herufi ***iI***<br>• Kadi za herufi kwa ajili ya marudio<br>• Kadi za maneno<br>• Andika neno ***[itika]*** ubaoni<br>• Kadi za sentensi<br>• Hadithi au Wimbo<br>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi |

## Muongozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 5)
## Marudio:

- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo: ***/m/,/a/,/k/***
- Uliza wanafunzi sauti ipi wanayosikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita (**Usiandike Maneno**). ***[alama, kitasa, madini]***

Fundisha sauti ***iI*** kwa kutumia muongozo ufuatao:

| Ujuzi | Mwalimu "Ninatenda" | Mwalimu na Mwanafunzi "tunatenda" *Rudia sauti zote na maneno* | Mazoezi ya mwanafunzi "unatenda" |
|---|---|---|---|
| **Utambuzi wa Sauti**<br><br>**(USIANDIKE)** | *Sauti mwanzo ya neno* ***[itika]*** *ni?* ***/i/*** *Sikiliza,* ***/iiii/***<br><br>*Sasa, sauti ya mwanzo ya neno* ***[imani]*** *ni?* ***/i/*** *Sikiliza,* ***/iiii/*** | *Sasa, tuseme sauti ya mwanzo neno* ***[itika]*** *Kilammoja, sauti ya mwanzo ya neno* ***[itika]*** *ni* ***/iiii/***<br>*Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe* (Haya sote tuseme) ***/iiii/***<br><br>*Sasa, fundisha sauti za mwanzo za neno* ***[imani]*** *kama ulivyofanya kwa* ***[itika]*** | **Mwalimu aulize:** Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia?<br>• ***Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wasichana wote, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wavulana wote, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Upande wangu wa kulia, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kulia)* *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto)* *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wote pamoja, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:* |

## Mazoezi ya utambuzi wa sauti

**Mchezo wa sauti:**

- Wambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao juu ya dawati wakati wa mchezo huu wa sauti.
- Wambie wanafunzi waoneshe dole gumba juu wanaposikia sauti ***/i/*** na dole gumba chini wasipoisikia sauti hiyo mwanzoni mwa maneno yafuatayo: (USIYAANDIKE) ***[mafuta, epua, ingia, timia, epuka, inama, elea, mapepe, itika]***

  Maana yake "Ndiyo" Maana yake "hapana"
- Ita mwanafunzi mmoja mmoja aseme neno linaloanza na sauti ***/i/.***
- Sahihisha makosa

## Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (Dakika 3-4)

**Marudio:**

- Rudia herufi ulizofundisha: ***m, a, k***
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie: **TAZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi ***m*** kisha waulize hiyo ni herufi gani
- Fanya hivyo kwa herufi ***a, k***
- Uliza wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja anafahamu majina ya herufi.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Msingi wa kialfabeti**<br><br>**Uhusiano wa Sauti na herufi**<br><br>**(ANDIKA)** | **Mwalimu: "Ninatenda" TAZAMA MAANDISHI.**<br><br>*Hii ni herufi **iI**.* Onesha wanafunzi herufi ***iI***. *Herufi **iI** inaunda sauti **/iiii/.*** | **Mwalimu na mwanafunzi: "Tunatenda"**<br><br>**TAZAMA MAANDISHI.**<br>*Sasa, kila mmoja: Hii ni herufi **iI**.* (Onesha wanafunzi herufi ***iI***) Herufi ***iI*** *inaunda sauti gani, sote kwa pamoja?* Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) ***/iiii/*** | **Mwalimu:**<br>*Sasa zamu yenu. Darasa hii ni herufi?* (Onesha herufi ***iI***)<br>• ***Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wasichana wote, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wavulana wote, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Upande wangu wa kulia, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kulia) Wanafunzi watasema:*<br>• ***Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto) Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wote pamoja, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:* |

**★ Mazoezi ya sauti ya herufi na ufasaha (4-5 dakika): MAZOEZI**

- Chukua kadi yenye herufi: ***iI*** (AU andika herufi hizo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi kisha onesha moja baada ya

nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.
**(Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii)**

- Tamka sauti ya herufi ***i/***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo.
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno ***[itika]*** ubaoni kisha sema "**Tazama maandishi**".
- Waoneshe namna ya kutamka (**Ninatenda, Tunatenda, Unatenda**). ***/i/ /t/ /i/ /k/ /a/***
- Unganisha sauti kisha sema neno ***[itika].***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno ***[itika],*** kisha watamke neno lote
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka maneno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kasha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke. (**Mnatenda**).
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno ***[itika]*** ni ***/iiii/,*** inayofuata ***/t/,*** inayofuata ***/iiii/,*** inayofuata ***/k/,*** *ya mwisho* ***/aaaa/.*** Neno gani hilo? ***[itika].*** Neno hilo ni ***[itika].***
- Sasa zamu yenu. Ni neno gani? ***[itika]***
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hiki. **(Ninatenda, Tunatenda, Unatenda)**

**Sentensi rahisi:**

- Sofia alipata ushindi wa Mwanafunzi aweze kusoma hadithi darasani.
- Ukiitwa jina lako itika.
- Mama aliepua chungu jikoni.
- Idadi kubwa ya watu ni wakulima.

**Mazoezi ya Kusoma Sentensi**

- Waoneshe wanafunzi kila herufi za sauti na utamke **[*Sofia aliibuka mshindi wa Mwanafunzi aweze kusoma hadithi darasani*].**
- Waambie wanafunzi wasome sentensi **kwa sauti**
- **Fanya hivyo kwa sentensi zilizosalia.**

## Msamiati: (Dakika 4-5)

RUDIA MANENO; ***[itika, inuka idadi, igiza]***

**Rejea neno la akiba:**

- Andika neno ***[itika]*** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa. Waambie walitumie katika sentensi kwa usahihi

**Neno jipya *[ya]*:**

- Waambie wanafunzi kuwa neno jipya lililotumiwa sana ni ***ya***
- Waoneshe kadi ya neno au liandike ubaoni.
- Waambie wanafunzi wasome neno pamoja na wewe.

**Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno; ***[itika, inuka idadi, igiza, ya]***

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Fanya hivyo kwa herufi ***a, o, p, w.***
- Uliza wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja anafahamu majina ya herufi.

Fundisha jina la herufi ***hH*** kutumia muongozo ufuatao

| **Kanuni za alfabeti**<br><br>**Uhusiano wa sauti na herufi**<br><br>**(ANDIKA)** | **Mwalimu "Ninatenda"**<br><br>*Hii ni herufi **hH.***<br>Onesha wanafunzi ***hH***.<br>*Herufi **hH** inaunda sauti **/h/.*** | **Mwalimu na mwanafunzi "Tunatenda"**<br><br>**TAZAMA MAANDISHI.**<br>*Sasa, kila mmoja: Hii ni herufi **hH**.* (Onesha wanafunzi herufi ***hH***) Herufi ***hH** inaunda sauti gani, sote kwa pamoja?*<br>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) ***/h/*** | **Mwanafunzi: "Unatenda"**<br>**Mwalimu:**<br>*Sasa zamu yenu. Darasa hii ni herufi?*<br>(Onesha herufi ***hH***)<br>• ***Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?***<br>*Wanafunzi watasema:*<br>• ***Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?***<br>*Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wasichana wote, sauti ipi?***<br>*Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wavulana wote, sauti ipi?***<br>*Wanafunzi watasema:*<br>• ***Upande wangu wa kulia, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kulia)*<br>*Wanafunzi watasema:*<br>• ***Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto)*<br>*Wanafunzi watasema:*<br>• ***Wote pamoja, sauti ipi?***<br>*Wanafunzi watasema:* |
|---|---|---|---|

## ★★Mazoezi ya sauti za herufi na ufasaha (4-5): MAZOEZI

- Chukua kadi za herufi ***rR*** (AU andika herufi ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi kisha onesha moja baada ya nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.
  **(Tumia sekunde 30 au zinazokaribiana kwa zoezi hili).**
- Sema sauti ya herufi ***rR***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema jina la herufi linalounda sauti hiyo.
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusema neno kwa kulitamka. Onesha neno [***hereni]*** kwenye ubao na useme **"Tazama Maandishi".**
- Waoneshe namna ya kutamka (**Natenda, Tunatenda, Unatenda**). ***/h/ /e/ /r/ /e/ /n/ /i/.***
- Unganisha sauti kisha sema neno [***hereni]***.
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno ***[hereni],*** kisha waseme neno lote.
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno.
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno *[**hereni]*** ni **/h /,** inayofuata **/eeee/,** inayofuata **/r/,** inayofuata **/eeee/,** inayofuta ***/n/*** ya mwisho ***/iiii/***. Neno gani? *[**hereni** ]* Neno hilo ni [***hereni]***
  Sasa zamu yenu. Neno gani? *[**hereni]***
- Onesha tena neno hilo kisha waambie wanafunzi walitamke kwa usahihi.
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno amabayo yamefundishwa katika kipindi hicho **(Natenda, Tunatenda, Mnatenda)**

**Sentensi rahisi:**

- Mama amevaa herini
- Utu wa mtu ni heshima
- Jana niliangalia taarifa ya habari kwenye TV
- Mimi ninawaheshimu walimu wangu
- Askari polisi wanatembea haraka

**Mazoezi ya Kusoma Sentensi.**

- Onesha kila herufi na uitamke kwa sauti ***[Mama amevaa hereni]***.
- Waambie wanafunzi wasome sentensi
- Kisha waambie wanafunzi wasome sentensi kwa sauti ukionesha kila neno**.**
- Fanya hivyo kwa sentensi zilizosalia

## Msamiati na maneno rejea: (Dakika 4-5)
Rudia maneno: *[**hereni, habari, hatari, hesabu**]*

**Neno la akiba:**

- Andika **hereni** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa hili ni neno la wiki.
- Waambie wanafunzi watumie neno hilo katika sentensi kwa usahihi.

**Neno jipya** *[**ni**]:*

- Waambie wanafunzi kuwa neno jipya la rejea ni *[**ni].***
- Onesha kadi au andika ubaoni.
- Waambie wanafunzi msome neno hilo pamoja.

**Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno [***hereni, haraka, hesabu, fahari]***

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonyesha (au onesha maneno hayo ubaoni).
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

## **Ufahamu wa kusikiliza** (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea yamekolezwa na yamepigiwa mstari.
Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wa Mwanafunzi aweze kusoma hadithi, tulia kwa muda na onesha msamiati huo ubaoni.

**Ufahamu**

Heshima ni kitu cha bure sana. Haihitaji gharama yoyote.
Watoto na wakubwa lazima waheshimiane. Baraka ni mtoto mwenye heshima.
Anawaheshimu wazazi wake na watu wote. Yeye no mfano kwa watoto wenziwe.

**Maswali ya ufahamu:**

- Heshima ni kitu gani?
- Kwanini watu wanaheshimiana?
- Je, heshima huwafanya watu wawe na tabia gani?
- Mtoto anatakiwa awaheshimu nani?

**Mazoezi:** Waambie wanafunzi wakatafute maneno yanayoundwa na ***/h/***

*Weka alama ya (√) baada ya kufundisha*

## 37.0 Marudio (Herufi kubwa na ndogo)
## Wiki ya 9: Siku ya 5

| | |
|---|---|
| Tarehe: ______________________<br>**Muongozo wa ufundishaji:** Tumia **jina la herufi/ sauti ya herufi** katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika<br>**Malengo:**<br>• Kufundisha sauti na jina la herufi ***wW, rR, hH*** kwa kutumia muongozo ufuatao<br>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma hadithi | **Zana:**<br>• Kadi mpya ya herufi **wW, rR, hH**.<br>• Kadi ya herufi kwa ajili ya marudiio<br>• Kadi za maneno:<br>• Andika neno ***[redio]*** ubaoni<br>• Kadi za sentensi<br>• Hadithi au wimbo<br>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi |

## Muongozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 5)

★ **Marudio**:
- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo **/w/, /r/, /h/**
- Uliza wanafunzi sauti ipi wanayoisikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita **(Usiandike Maneno**).

Rudia sauti ***wW, rR, hH*** kwa kutumia muongozo ufuatao:

| Ujuzi | Mwalimu "Natenda" | Mwalimu na mwanafunzi "Tunatenda" *Rudia sauti zote na maneno* | Mazoezi ya mwanafunzi "Unatenda" |
|---|---|---|---|
| **Utambuzi wa Sauti**<br><br>**(USIANDIKE)** | *Mwalimu aongoze kutambua sauti za mwanzo za maneno tofauti kutoka masomo yaliyotangulia.* | *Sasa, Tuseme sauti ya mwanzo kutoka katika maneno tofauti tuliyojifunza somo lililopita* | **Mwalimu aulize:** Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia?<br>• ***Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?***<br>*Wanafunzi watasema:*<br>• ***Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Wasichana wote, sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Wavulana wote sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kulia, sauti ipi?*** *(mwalinu elekeza mkono upande wa kulia)*<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto*<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Wote kwa pamoja, sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema: |

## Mazoezi ya Utambuzi wa Sauti

**Mchezo wa Sauti:**

- Waambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao kwenye madawati (USIYAANDIKE)
- Sahihisha makosa

## Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 3-4)

**Marudio:**

- Rudia herufi zilizokwisha fundishwa: ***wW, rR, hH***
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie: **TAZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi ***wW*** kisha waulize hiyo ni herufi gani
- Fanya hivyo kwa herufi ***rR, hH***
- Uliza wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja anafahamu majina ya herufi.

Rudia majina ya herufi ***wW, rR, hH*** kutumia muongozo ufuatao

| Kanuni za alfabeti | Mwalimu: "Ninatenda" | Mwalimu na mwanafunzi: "Tunatenda" | Mwanafunzi: "Unatenda" |
|---|---|---|---|
| **Uhusiano wa Sauti na herufi**<br><br>**(ANDIKA)** | **TAZAMA MAANDISHI.**<br>*Hii ni herufi **wW**.* Onesha wanafunzi **wW**. Herufi *wW inaunda sauti /**w**/.*<br><br>*Hii ni herufi **rR**.* (Onesha wanafunzi **rR**). *Herufi **rR** inaunda sauti **/rrrr/.***<br><br>*Hii ni herufi **hH**.* Onesha wanafunzi ***hH***. *Herufi **hH** inaunda sauti **/h/.*** | **TAZAMA MAANDISHI.**<br>*Kila mmoja: hii ni sauti **wW**.* (Onesha **wW**.) *Herufi **wW** inaunda sauti gani,. . . kila mmoja?*<br>Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (darasa zima) ***/w/***<br><br>Sasa kila mmoja: hii ni herufi ***rR***. (Onesha wanafunzi herufi ***rR***.) Herufi ***rR*** inaunda sauti? Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (Darasa zima) ***/rrrrr/***<br><br>*Sasa, kila mmoja: hii ni herufi **hH**.* (Onesha wanafunzi ***hH***.) *Herufi hH inaunda sauti gani, sote?*<br>Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (darasa zima) ***/h/*** | Mwalimu wagawie wanafunzi kadi za maneno katika makundi na waambie wachague herufi zinazoashiria sauti zilizotamkwa |

**★★ Mazoezi ya Sauti ya herufi na ufasaha (Dakika 4-5): MAZOEZI**

- Chukua kadi zenye herufi ***wW, rR, hH,*** (AU andika herufi hizo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi kisha onesha moja baada ya

nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.
**(Tumia sekunde 30 au zinazokaribiana kwa zoezi hili).**

- Sema sauti ya herufi ***wW***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema jina la herufi linalounda sauti hiyo. Fanya hivyo kwa herufi: ***rR, hH***
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusema neno kwa kulitamka. Onesha neno [watoto, wazee, ***hereni, redio]*** kwenye ubao na useme **"Tazama Maandishi".**

- Waoneshe namna ya kutamka (**Natenda, Tunatenda, Unatenda**)***/w/ /a/ /t/ /o/ / t/ /o/***
- Unganisha sauti kisha sema neno ***[watoto]***.
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika ***[watoto]***, kisha waseme neno lote.
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno [***watoto]*** ni **/w /,** inayofuata **/aaaa/,** inayofuata **/t/,** inayofuata **/oooo/,** inayofuata ***/t/***, ya mwisho ni **/oooo/**. Neno gani? [***watoto*** ] Neno hilo ni ***[watoto]***
- Sasa zamu yenu. Neno gani? ***[watoto]***
- Onesha tena neno hilo kisha waambie wanafunzi walitamke kwa usahihi.
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno amabayo yamefundishwa katika kipindi hicho **(Natenda, Tunatenda, Mnatenda)**

**Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia [***watoto, redio, wazee, ramani, hereni, fahari, mawazo***, ***kiroba, hesabu]***

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonyesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua.
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

## Msamiati: (Dakika 4-5)

RUDIA Maneno *[**hekima, redio, hereni, hesabu, wazee, watoto]***

## Ufahamu wa kusikiliza (Dakika 10):

- Wasomee wanafunzi hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno

yamekolezwa na yamepigiwa mstari

- Yaandike maneno ubaoni. Tulia kwa muda kisha waoneshe unapoyatamka

## Hadithi ya Kusoma kwa Sauti [Jina la Hadithi]

- Andika jina la hadithi ubaoni
- Andika jina la mwandishi
- Andika jina la msanifu wa michoro.

**Rejea neno la akiba:**

- Andika neno ***[redio]*** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa. Waambie walitumie katika sentensi
- Waambie wanafunzi wayatumie maneno hayo kwa ufasaha.

*Weka alama ya (√) baada ya kufundisha*

## 38.0 Kufundisha herufi vV
## Wiki ya 10: Siku ya 1

| | |
|---|---|
| Tarehe: ___________________________<br>**Muongozo wa ufundishaji:** Tumia **jina la herufi/ sauti ya herufi** katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika.<br>**Malengo:**<br>• Kufundisha sauti na jina la herufi ***vV*** kwa kutumia muongozo ufuatao<br>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma hadithi | **Zana:**<br>• Kadi ya herufi ***vV***.<br>• Kadi ya herufi kwa ajili ya marudio:<br>• Kadi za maneno<br>• Andika neno ***[vitabu]***<br>• Kadi za sentensi<br>• Hadithi au wimbo<br>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi |

## Muongozo wa kufundisha Utambuzi wa Sauti (Dakika 5)

★ **Marudio**:

- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo: ***/r/, /a/, /o/, /h/, /w/***
- Uliza wanafunzi sauti ipi wanayosikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lililopita **(Usiandike Maneno)** ***[asali, watoto, hereni, ramani, walimu, ogopa, hesabu]***

Fundisha sauti ***vV*** kwa kutumia muongozo ufuatao:

| Ujuzi | Mwalimu “Natenda” | Mwalimu na Wanafunzi “Tunatenda” *Rudia sauti zote na maneno* | Mazoezi ya Mwanafunzi “Mnatenda” |
|---|---|---|---|
| Utambuzi wa Sauti<br><br>**(USIANDIKE)** | *Sauti mwanzo ya neno **[vitabu]** ni? **/v/** Sikiliza, **/v/***<br><br>*Sasa, sauti ya mwanzo ya neno **[vuruga]** ni? **/v/** Sikiliza, **/v/*** | *Sasa, tuseme sauti ya mwanzo neno **[vitabu]** Kilammoja, sauti ya mwanzo ya neno **[vitabu]** ni **/v/***<br><br>Mwalimu awaongoze wanafunzi kutamka sauti kwa kunyanyua mkono na kushusha akisema. (Haya sote tuseme) ***/v/***<br><br>*Sasa, fundisha sauti ya mwanzo ya neno **[vuruga]** kama ulivyofanya kwa **[vitabu]*** | **Mwalimu aulize:** Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia? (Rejea maneno ya ma |

## Mazoezi ya Utambuzi wa Sauti

**Mchezo wa Sauti:**

- Waambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao juu ya dawati wakati wa mchezo huu wa sauti.
- Waambie wanafunzi waoneshe dole gumba juu wanaposikia sauti ***/v/*** na dole gumba chini wasipoisikia sauti hiyo mwanzoni mwa maneno yafuatayo: (USIYAANDIKE): **[vuruga, hesabu, mawazo, vitani, redio, vurugu, refusha, kiroba, vitabu]**

Maana yake **“ndiyo**” Maana yake **“hapana”**

- Ita mwanafunzi mmoja mmoja aseme neno linaloanza na sauti ***/v/.***
- Sahihisha makosa

## Muongozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 3-4)

**Marudio:**

- Rudia herufi zilizokwisha fundishwa: ***w, r, m, a, k, o, t, p***
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie **TAZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi ***m*** kisha waulize hiyo ni herufi gani.
- Fanya hivyo kwa herufi zingine.
- Uliza wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja anafahamu majina ya herufi.

Fundisha jina la herufi ***vV*** kutumia muongozo ufuatao

| Kanuni za alfabeti (ANDIKA) | Mwalimu "Natenda" | Mwalimu na Mwanafunzi "Tunatenda" | Wanafunzi " Unatenda" |
|---|---|---|---|
| | *Hii ni herufi **v**.* Onesha wanafunzi herufi ***vV***. *Herufi **vV** inaunda sauti* **/v/.** | *Sasa, kila mmoja: Hii ni herufi **vV**.* (Onesha wanafunzi herufi ***vV***) Herufi ***vV** inaunda sauti gani, sote kwa pamoja?* Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) ***/v/*** | **Mwalimu atasema:** *Sasa zamu yenu. Wanafunzi ni herufi gani?* (Onesha ***vV***) **Tazama Maandishi.** |

## ★★ Mazoezi ya sauti ya herufi na ufasaha (Dakika 4-5): MAZOEZI

- Chukua kadi yenye herufi ***vV*** (AUziandike ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la herufi, kisha onesha moja baada ya nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo. **(Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii).**
- Tamka sauti ya herufi ***vV***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo.
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno ***[vitabu]*** ubaoni kisha sema **"Tazama Maandishi."**
- Waoneshe namna ya kutamka (**Natenda, Tunatenda, Mnatenda**). ***/v/ /i/ /t /a/ /b/ /u/.***
- Unganisha sauti kisha sema neno ***[vitabu]***.
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno ***[vitabu]*** kisha watamke neno lote.
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.i zinazounda neno
- Onesha neno kisha tamka sau
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke **(Mnatenda)**.
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya mwanzo katika neno **vitabu** ni ***/v /***, inayofuata ***/iiiii/***, inayofuata ***/t/,*** inayofuata ***/ aaaa***/, inayofuata ***/b/***, ya mwisho ni ***/uuuu***/. Neno gani hilo? [***vitabu]*** Neno hilo ni? [***vitabu]***
- Sasa zamu yako. Ni neno gani? [***Vitabu]***
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hiki. **(Ninatenda, Tunatenda, Unatenda)**

**Sentensi rahisi:**

- Mimi ninapenda kuvaa kofia

- Kaka anapenda kuvua samaki
- Watanzania hwapendi vurugu
- Vaa nguo zako uende shule
- Watoto wanapenda vitabu vya hadithi.

**Mazoezi ya Sentensi.**

- Waoneshe wanafunzi kila herufi za sauti na utamke *[**Watoto wanapenda vitabu vya hadithi]***.
- Kisha waambie wanafunzi wasome sentensi kwa sauti.
- Fanya hivyo kwa sentensi zilizosalia

## Msamaiati: (Dakika 4-5)

RUDIA MANENO: [v***itabu, vuruga, vutia, vamia, valia]***

**Rejea neno la akiba:**

- Andika neno [***vitabu]*** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limeshafundishwa. Waambie walitumie katika sentensi kwa usahihi.

**Neno jipya** [***kwa]***:

1. Waambie wanafunzi kuwa neno jipya lililotumiwa sana ni [***kwa]***.

- Waoneshe kadi ya neno au liandike ubaoni
- Waambie wanafunzi wasome neno hilo pamoja na wewe.

**Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno ***[v**itabu, hereni, vuruga, vutia, vamia, wazee, valia]***

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, kwa hiyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

**Ufahamu wa kusikiliza** (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO Msamiati na maneno rejea yamekolezwa na yamepigiwa mstari. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kusoma hadithi, tulia kwa muda na onesha msamiati huo ubaoni.

**Ufahamu**

Hesabu ni nzuri sana ee
Hesabu ni nzuri sana ee
Mwalimu nifundishe, nipate kuhesabu
Ee Mwalimu, ee mwalimu nifundishe

**Maswali ya Ufahamu**

- Mwalimu atakufundisha nini?
- Kwanini hesabu ni nzuri?
- Taja masomo tunayojifunza shuleni
- Hesabu namba moja hadi kumi
- Je, unapenda kuwa mwalimu wa hesabu?

**Mazoezi:**

Waambie wanafunzi watafute maneno yanayoanza na sauti /**v/**

*Weka alama ya (√) baada ya kufundisha*

## 39.0 Kufundisha herufi thTH
## Wiki ya 10: Siku ya 2.

| | |
|---|---|
| Tarehe: ____________________<br>**Muongozo wa ufundishaji:** Tumia **jina la herufi/sauti ya herufi** katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika<br>**Malengo:**<br>• Kufundisha sauti na jina la herufi ***thTh*** kwa kutumia muongozo ufuatao<br>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma hadithi | **Zana:**<br>• Kadi ya herufi ***thTh***.<br>• Kadi ya herufi kwa ajili ya marudio:<br>• Kadi za maneno<br>• Andika neno ***[theluji]***<br>• Kadi za sentensi<br>• Hadithi au wimbo<br>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi |

**Muongozo wa kufundisha** utambuzi wa sauti (Dakika 5)

★ **Marudio**:

- Rudia sauti zilizofundishwa katika wiki hiyo: ***/h/ /a/, /k/, /o/, /w/, /v/***
- Uliza wanafunzi sauti ipi wanayosikia mwanzoni mwa kila neno lilofundishwa katika somo lililopita: [***vurugu, watoto, vamia, mawazo, samaki, walimu, tikisa, zaliwa, watatu].***

Fundisha sauti ***thTh*** kwa kutumia muongozo ufuatao:

| **Ujuzi** | **Mwalimu "Ninatenda"** | **Mwalimu na mwanafunzi "Tunatenda"** *Rudia sauti zote na maneno* | **Mazoezi ya mwanafunzi "Unatenda"** |
|---|---|---|---|
| Utambuzi wa Sauti<br><br>**(USIANDIKE)** | *Sauti mwanzo ya neno [**theluji]** ni **/th/** Sikiliza **/th/**.*<br><br>*Sasa, sauti ya mwanzo ya neno **[theluthi]** ni? **/th/** Sikiliza, **/th/*** | *Sasa, tuseme sauti ya mwanzo ya neno [**theluji]** pamoja. Kila mmoja, sauti ya mwanzo ya neno [**theluji]** ni **/th/***<br><br>Mwalimu awaongoze wanafunzi kutamka sauti kwa kunyanyua mkono na kushusha akisema. (Haya sote tuseme) ***/th/***<br><br>*Sasa, fundisha sauti ya mwanzo ya neno **[theluthi]** kama ulivyofanya kwa **[theluji]*** | **Mwalimu aulize:** Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia?<br>• ***Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Wasichana wote, sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Wavulana wote sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kulia, sauti ipi?*** *(mwalinu elekeza mkono upande wa kulia)* Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto* Wanafunzi watasema:<br>• ***Wote kwa pamoja, sauti ipi?*** Wanafunzi watasema: |

## Mazoezi ya utambuzi wa sauti

**Mchezo wa sauti:**

- Wambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao juu ya dawati wakati wa mchezo huu wa sauti.
- Wambie wanafunzi waoneshe dole gumba juu wanaposikia sauti ***/m/*** na dole gumba chini wasipoisikia sauti hiyo mwanzoni mwa maneno yafuatayo: (USIYAANDIKE): ***[themanini, watoto, samani, mawazo, thumni, pakia, thamani, ramani, dhumuni, kiroba, theluji, nanasi]***

  Maana yake "Ndiyo" Maana yake "Hapana"
- Ita mwanafunzi mmoja mmoja aseme neno linaloanza na sauti ***/th/.***
- Sahihisha makosa

## Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (Dakika 3-4)

**Marudio:**

- Rudia herufi zilizokwisha fundishwa: ***k, i, w, a, o, v***
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. **TAZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi ***k*** kisha waulize hiyo ni herufi gani.
- Fanya hivyo kwa herufi zingine
- Uliza wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja anafahamu majina ya herufi.

Fundisha majina ya herufi ***thTh*** kutumia muongozo ufuatao:

| Kanuni za alfabeti<br><br>Uhusiano wa sauti na herufi<br><br>(ANDIKA) | Mwalimu "Ninatenda"<br><br>TAZAMA MAANDISHI<br><br>*Hii ni herufi **thTh**.* Onesha wanafunzi herufi ***thTh**. Herufi* ***thTh*** *inaunda sauti* ***/th/.*** | Mwalimu na mwanafunzi: "Tunatenda"<br><br>*Sasa, kila mmoja: hii ni herufi **thTH**.* (Onesha ***thTh***) *Herufi **thTh** inaunda sauti?* Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (sote tuseme) ***/th/*** | **Mwanafunzi " Unatenda"**<br>*Sasa zamu yenu. Darasa hii ni herufi?* (Onesha herufi ***thTh***)<br>**TAZAMA MAANDISHI**<br>• ***Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?***<br>*Wanafunzi watasema:*<br>• ***Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Wasichana wote, sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Wavulana wote sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kulia, sauti ipi?*** *(mwalinu elekeza mkono upande wa kulia)*<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto*<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Wote kwa pamoja, sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema: |
|---|---|---|---|

## ★★ Mazoezi ya sauti ya herufi na ufasaha (Dakika 4-5): MAZOEZI

- Chukua kadi yenye herufi ***thTh*** (AU andika ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi, kisha onesha moja baada ya nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.
  **(Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii).**
- Tamka sauti ya herufi ***th***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo. Fanya hivyo kwa herufi: ***k, l, w, a, o, v***
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kulisema neno kwa kulitamka. Onesha neno [***theluthi]*** ubaoni kisha sema neno. Kisha sema **"Tazama Maandishi."**
- Waoneshe namna ya kutamka (**Natenda, Tunatenda, Mnatenda**) ***/th/ /e/ /l/ /u/ / th/ /i/.***
- Unganisha sauti kisha sema neno [***theluthi]***.
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno ***[theluthi]*** kisha watamke neno lote.
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke (Mnatenda).
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya kwanza katika neno **[theluthi]** ni ***/th /***, inayofuata ***/eeee/***, inayofuata ***/l/,*** inayofuata

***/uuuu***/, inayofuata ***/th/***, ya mwisho ni ***/iiii***/. Neno gani hilo? [***theluthi]*** Neno hilo ni [***theluthi]***

- Sasa zamu yenu. Ni neno gani? [***theluthi]***
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno ambayo yamefundishwa katika kipindi hiki. **(Ninatenda, Tunatenda, Unatenda)**

**Sentensi rahisi:**

- Mimi nina vihesabio thelathini.
- Juma alithubutu kugombana na baba yake.
- Thamani ya kijana ni kazi
- Mlima Kilimanjaro umefunikwa na theluji
- Babu yangu ana miaka themanini.

**Mazoezi ya Kusoma Sentensi**

- Waoneshe wanafunzi kila herufi za sauti na utamke [***Mimi nina vihesabio thelethini].***
- Waambie wanafunzi wasome sentensi kwa sauti**.**
- Fanya hivyo kwa sentensi zilizosalia

## Msamiati: (Dakia 4-5)

Marudio: ***[theluji, thamani, thelethini, theluthi]***

**Neno la akiba:**

- Andika [**theluji]** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa. Waambie wanafunzi walitumie neno hili kwa usahihi katika sentensi.

**Neno Jipya** [***kwa]***:

- Waambie wanafunzi kuwa neno jipya lililotumiwa sana ni ***kwa***.
- Waoneshe kadi ya neno (au liandike ubaoni).
- Waambie wanafunzi wasome neno pamoja na wewe.

**Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno; [***theluji, thamani, thelethini, theluthi***]

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, hivyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

**Ufahamu wa kusikiliza** (Dakika 10):
Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea yamekolezwa na yamepigiwa mstari. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kusoma hadithi, tulia kwa muda na onesha msamiati huo ubaoni.

## Ufahamu:

Mimi ni theluthi napatikana katika heabu za sehemu. Ukichukuwa chungwa ukikata vipande vitatu kipande kimoja kinaitwa theluthi. Mimi nimempa rafiki yangu theluthi ya chumgwa langu.

**Maswali ya ufahamu:**

- Mimi ni nani?
- Theluthi inapatikana wapi?
- Ukikata vipande vingapi unapata theluthi?
- Nilimpa nini rafiki yangu?

**Mazoezi:**

Waambie wanafunzi watafute maneno yanayoanza na sauti **/th/**

*Weka alama ya (√) baada ya kufundisha*

## 40.0 Kufundisha herufi shSh
## Wiki ya 10: Siku ya 4.

| | |
|---|---|
| Tarehe: ________________________<br>**Muongozo wa ufundishaji:** Tumia **jina la herufi/sauti ya herufi** katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika<br>**Malengo:**<br>• Kufundisha sauti na jina la herufi ***shSh*** kwa kutumia muongozo ufuatao<br>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma hadithi | **Zana:**<br>• Kadi ya herufi ***shSh***.<br>• Kadi ya herufi kwa ajili ya marudio:<br>• Kadi za maneno<br>• Andika neno ***[shangazi]***<br>• Kadi za sentensi<br>• Hadithi au wimbo<br>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi |

## Mwomgozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 5)

★ **Marudio**:

- Rudia sauti zilizofundishwa: ***/th/, /v/, /a/, /k/, /o/, /i/***
- Uliza wanafunzi sauti ipi wanayosikia mwanzoni mwa kila neno: ***[thelathini, vamia, vurugu, alama, amani, kalamu, okota, inama].***

Fundisha sauti ***shSh*** kwa kutumia muongozo ufuatao:

| **Ujuzi** | **Mwalimu**<br>**"Natenda"** | **Mwalimu na Wanafunzi**<br>**"Tunatenda"**<br>*Rudia sauti zote na maneno* | **Mazoezi kwa mwanafunzi**<br>**"Unatenda"** |
|---|---|---|---|
| Kanuni za alfabeti<br><br>**(USIANDIKE)** | *Sauti mwanzo ya neno **[shangazi]** ni* ***/sh/*** Sikiliza ***/shhh/***.<br><br>*Sasa, sauti ya mwanzo ya neno **[shuleni]** ni?* ***/sh/*** *Sikiliza,* ***/shhh/*** | *Sasa, tuseme sauti ya mwanzo ya neno **[shangazi]** pamoja. Kila mmoja, sauti ya mwanzo ya neno **[shangazi]** ni **/sh/***<br><br>Mwalimu awaongoze wanafunzi kutamka sauti kwa kunyanyua mkono na kushusha akisema. (Haya sote tuseme) ***/shhh/***<br><br>*Sasa, fundisha sauti ya mwanzo ya neno **[shuleni]** kama ulivyofanya kwa **[shangazi]*** | **Mwalimu aulize:** Ni sauti gani ya mwanzo mnayoisikia?<br>• ***Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?***<br>*Wanafunzi watasema:*<br>• ***Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Wasichana wote, sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Wavulana wote sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kulia, sauti ipi?***<br>*(mwalinu elekeza mkono upande wa kulia)*<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?***<br>*(mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto*<br>Wanafunzi watasema:<br>• ***Wote kwa pamoja, sauti ipi?***<br>Wanafunzi watasema: |

## Mazoezi ya Utambuzi wa sauti

**Mchezo wa sauti**

- Wambie wanafunzi wainamishe vichwa vyao juu ya dawati wakati wa mchezo huu wa sauti.
- Wambie wanafunzi waoneshe dole gumba juu wanaposikia sauti ***/sh/*** na dole gumba chini wasipoisikia sauti hiyo mwanzoni mwa maneno yafuatayo: (USIYAANDIKE): ***[themanini, dirisha, shambani, rashidi, shangazi, mawazo, sherehe, pakia, dhumuni, shetani, theluji]***

  Maana yake "Ndiyo"  Maana yake "Hapana"
- Ita mwanafunzi mmoja mmoja aseme neno linaloanza na sauti **/sh/**.
- Sahihisha makosa

## Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti ya herufi (Dakika 3-4)

**Rudia:**

- Rudia herufi zilizokwisha fundishwa: **th, *v, k, i, a, o***
- Andika herufi ubaoni au tmia kadi za herufi. **TAZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi ***th*** kisha waulize hiyo ni herufi gani.
- Fanya hivyo kwa herufi zingine.
- Uliza wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja anafahamu majina ya herufi.

Fundisha majina ya herufi ***shSh*** kutumia muongozo ufuatao

| **Kanuni za alphabeti**<br><br>**Utambuzi wa Sauti**<br><br>**(ANDIKA)** | **Mwalimu "Natenda"**<br><br>Hii ni herufi ***shSh.*** Onesha wanafunzi ***shSh***. *Sauti* ***shSh*** *inaunda* ***/sh/***. | **Mwalimu na wanafunzi "Tunatenda"**<br><br>*Sasa, tuseme sauti ya mwanzo: Hii ni sauti* ***shSh.*** (Onesha wanafunzi herufi ***shSh***). *Herufi* ***shSh*** *inaunda sauti gani, sote?*<br><br>Onesha ishara kwa mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja nawe. (haya tuseme) **/sh/** | **Wanafunzi " Unatenda"**<br>*Sasa zamu yenu. Darasa hii ni herufi?* (Onesha herufi ***shSh***)<br>**TAZAMA MAANDISHI**<br>• ***Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Wasichana wote, sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Wavulana wote sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kulia, sauti ipi?*** *(mwalinu elekeza mkono upande wa kulia)* Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto* Wanafunzi watasema:<br>• ***Wote kwa pamoja, sauti ipi?*** Wanafunzi watasema: |
|---|---|---|---|

## ★★ Mazoezi ya sauti ya herufi na ufasaha (Dakika 4-5): MAZOEZI

- Chukua kadi zenye herufi ***shSh*** (AU andika herufi hizo ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi, kisha onesha moja baada ya nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.
  **(Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii).**
- Tamka sauti ya herufi ***shSh***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo. Fanya hivyo kwa herufi: **th, v, k, l, a, o**
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kusoma neno kwa kulitamka. Onesha neno ***[shangazi]*** ubaoni kisha sema **"Tazama Maandishi."**
- Waoneshe namna ya kutamka (**Natenda, Tunatenda, Mnatenda**). ***/sh/ /a/ /ng//a/ /z/ /i/.***
- Unganisha sauti kisha sema neno ***[shangazi]***.
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno ***[shangazi]*** kisha watamke neno hilo.
- Uliza wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke **(Mnatenda)**.
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya kwanza katika neno [**shangazi]** ni ***/sh /***, inayofuata ***/aaaa/***, inayofuata ***/ng/,***

inayofuata ***/aaaa***/, inayofuata ***/z/***, ya mwisho ni ***/iiii***/. Neno gani hilo? ***[shangazi]*** Neno hilo ni ***[shangazi]***

- Sasa zamu yenu. Ni neno gani? [***shangazi]***
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno katika kipengele cha (**Natenda, Tunatenda, Unatenda**)

**Sentensi rahisi:**

- Shangazi anauza vitumbua sokoni.
- Watoto huvaa nguo nzuri siku za sherehe.
- Mwalimu Nyerere ni shujaa wa Tanzania
- Kila siku asubuhi mimi nikaula vitumbua
- Shule yetu ina mashimo matatu ya takataka

**Mazoezi ya Kusoma Sentensi:**

- Waoneshe wanafunzi kila herufi za sauti na utamke ***[Shangazi anauza vitumbua sokoni]***.
- Waambie wanafunzi wasome sentensi kwa sauti**.**
- Fanya hivyo kwa sentensi zilizosalia

## Misamiati: (Dakika 4-5)

RUDIA MANENO: ***[shambani, shangazi, sherehe, shuleni,]***

**Neno la akiba:**

- Andika neno **[shangazi]** ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa hili ni neno la wiki.
- Waambie wanafunzi walitumie neno hili kwa usahihi katika sentensi.

**Neno jipya** [***kwa]***:

- Waambie wanafunzi kuwa neno jipya lililotumiwa sana ni [***kwa]***.
- Waoneshe kadi ya neno au liandike ubaoni.
- Waambie wanafunzi wasome neno pamoja na wewe.

**Mchezo wa kujenga ufasaha** kutumia maneno ***[shambani, shangazi, sherehe, shuleni***]

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, hivyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

**Ufahamu wa kusikiliza** (Dakika 10):

Wasomee hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea yamekolezwa

na yamepigiwa mstari. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kusoma hadithi, tulia kwa muda na onesha msamiati huo ubaoni.

**Ufahamu**

Shangazi yangu anapika vitumbua. Sofia huamka asubuhi na kwenda kuviuza sokoni. Huuza kitumbua kimoja kwa shilingi hamsini. Watu wengi wanavipenda vitumbua kwa sababu ni vitamu sana.

**Maswali ya Ufahamu:**

- Shangazi anapika nini?
- Kwanini shangazi anapika vitumbua?
- Vitumbua vinauzwa wapi?
- Vitumbua hupikwa kwa kutumia nini?

**Mazoezi:** Waambie wanafunzi watafute maneno yanayoanza ***/sh/***

*Weka alama ya (√) baada ya kufundisha*

## 41.0 Marudio ya herufi kubwa na ndogo
## Wiki ya 10: Siku ya 5

| | |
|---|---|
| Tarehe: ______________________<br>**Muongozo wa ufundishaji:** Tumia **jina la herufi/sauti ya herufi** katika muongozo huu ili kufundisha majina na sauti za herufi husika<br>**Malengo:**<br>• Kufundisha sauti na jina la herufi ***vV, thTh, shSh*** kwa kutumia muongozo ufuatao<br>• Mwanafunzi aweze kufanya mazoezi ya kusoma kwa kutumia kadi za herufi, maneno na sentensi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma sentensi rahisi<br>• Mwanafunzi aweze kusoma hadithi | **Zana:**<br>• Kadi ya herufi ***vV, thTh, shSh***.<br>• Kadi ya herufi kwa ajili ya marudio:<br>• Kadi za maneno<br>• Andika neno ***[shangazi]***<br>• Kadi za sentensi<br>• Hadithi au wimbo<br>• Kitini cha mazoezi kwa mwanafunzi |

## Muongozo wa kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 5)

★ **Marudio**:

- Rudia sauti zilizofundishwa: ***vV, thTh, shSh***
- Uliza wanafunzi sauti ipi wanasikia mwanzoni mwa kila neno lililofundishwa katika somo lilopita (**USIANDIKE maneno**).

Rudia sauti kwa kutumia muongozo ufuatao.

| Ujuzi | Mwalimu "Natenda" | **Mwalimu na mwanafuzi "tunatenda"** *Rudia sauti zote za mwanzo* | Mazoezi ya mwanafunzi "Unatenda" |
|---|---|---|---|
| **Utambuzi wa sauti**<br><br>**(USIANDIKE)** | *Mwalimu aongoze kutambua sauti za mwanzo za maneno tofautikutoka masomo yaliyotangulia.* | *Sasa, Tuseme sauti ya mwanzo kutoka katika maneno tofauti tuliyojifunza somo lililopita* | **Mwalimu aulize:** Ni sauti gani ya mwanzo mnayosikia (Rejea maneno ya masomo yaliyopita)<br>• ***Mistari mitatu ya nyuma, sauti ipi?*** *Wanafunzi watasema:*<br>• ***Mistari mitatu ya mbele, sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Wasichana wote, sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Wavulana wote sauti ipi?*** Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kulia, sauti ipi?*** *(mwalinu elekeza mkono upande wa kulia)* Wanafunzi watasema:<br>• ***Upande wangu wa kushoto, sauti ipi?*** *(mwalimu elekeza mkono upande wa kushoto* Wanafunzi watasema:<br>• ***Wote kwa pamoja, sauti ipi?*** Wanafunzi watasema: |

## Mazoezi ya utambuzi wa sauti

**Mchezo wa sauti:**

- Waambie wanafunzi wasimame wanaposikia sauti ya mwanzo ya maneno waliyojifunza (USIYAANDIKE)
- Sahihisha makosa

## Maelekezo ya kufundisha utambuzi wa sauti (Dakika 3-4)

**Marudio:**

- Rudia herufi zilizokwisha fundishwa: ***vV, thTh, shSh***
- Andika herufi ubaoni au tumia kadi za herufi. Waambie **TAZAMA MAANDISHI.**
- Waoneshe wanafunzi kadi ya herufi ***vV*** kisha waulize hiyo ni herufi gani.
- Fanya hivyo kwa herufi zingine.
- Uliza wanafunzi kadhaa kuhakikisha kila mmoja anafahamu majina ya herufi.

Rudia majina ya herufi ***vV, thTh, shSh*** kwa kutumia muongozo ufuataoa.

| Kanuni za alfabeti<br><br>Utambuzi wa sauti<br><br>(ANDIKA) | Mwalimu: Natenda<br>TAZAMA MAANDISHI.<br>*Hii ni herufi **vV**.* Onesha wanafunzi ***vV**. Herufi **vV** inaunda sauti **/v/.***<br><br>*Hii ni herufi **thTh**.* (Onesha wanafunzi ***thTh***).*Herufi **thTh** inaunda sauti **/th/.***<br><br>*Hii ni herufi **shSh**.* Onesha wanafunzi ***shSh**. Herufi **shSh** inaunda sauti **/sh/.*** | Mwalimu na Wanafunzi: Tunatenda<br>TAZAMA MAANDISHI.<br>*Kila mmoja: Hii ni sauti **vV**.* (Onesha wanafunzi ***vV***). *Sauti **vV** inatoa sauti gani, kila mmoja?* Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (darasa zima) ***/v/***<br><br>Sasa Kila mmoja: Hii ni herufi **thTh**. (Onesha wanafunzi herufi **thTh**). Herufi **thTh** inaunda sauti gani, kila mmoja?<br>Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (darasa zima) **/th/**<br><br>*Sasa, kila mmoja: hii ni herufi **shSh**.* (Onesha wanafunzi **shSh**). *Herufi **shSh** inaunda sauti gani?*<br>Nyoosha mkono kuashiria wanafunzi wajibu pamoja na wewe. (darasa zima) **/shhh/** | Wanafunzi: Unatenda<br><br>Mwalimu wagawie wanafunzi kadi za herufi katika makundi na waambie wachague herufi zinazoendana na sauti zilizotankwa |
|---|---|---|---|

**★★ Mazoezi ya sauti ya ufasaha na ufasaha (Dakika 4-5): MAZOEZI**

- Chukua kadi zenye herufi **v, th, sh** (AU ziandike ubaoni).
- Wakumbushe wanafunzi jina la kila herufi, kisha onesha moja baada ya nyingine huku ukiwataka wanyooshe mkono kama wanajua majina ya herufi hizo.
  **(Tumia sekunde 30 au zaidi kwa kazi hii).**
- Tamka sauti ya herufi ***shSh***
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kutaja jina la herufi linalounda sauti hiyo. Fanya hivyo kwa herufi: **vV, thTh**
- Waulize wanafunzi kama wanaweza kulisema neno kwa kulitamka. Onesha neno [***vitabu]*** ubaoni kisha sema **"Tazama Maandishi."**
- Waoneshe namna ya kutamka (**Natenda, Tunatenda, Mnatenda**).***/v/ /i/ /t/ /a/ /b/ /u/.***
- Unganisha maneno kisha sema neno ***[vitabu]***.
- Waambie wanafunzi wanyooshe mkono kama wanaweza kusema sauti zilizopo katika neno ***[vitabu]*** kisha watamke neno lote.
- Chagua wanafunzi kadhaa kutamka neno hilo.
- Sahihisha makosa.
- Onesha neno kisha tamka sauti zinazounda neno
- Onesha neno kisha waambie wanafunzi walitamke (Mnatenda).
- Onesha kila herufi kisha tamka pamoja na wanafunzi. Sauti ya kwanza katika neno **vitabu** ni ***/v /***, inayofuata ***/iiii*** , inayofuata ***/t/,*** inayofuata ***/aaaa***/,

inayofuata ***/b/***, ya mwisho ni ***/uuuu***/. Neno gani hilo? ***[vitabu]*** Neno hilo ni ***[vitabu]***

- Sasa zamu yenu. Ni neno gani? [***vitabu]***
- Waambie wanafunzi waandike herufi mpya, silabi na maneno katika kipengele cha (**Natenda, Tunatenda, Unatenda**)

**Mchezo wa kujenga** ufasaha kutumia maneno***; [vitabu, vurugu, viatu, theluji, thelathini, theluthi, shangazi, shujaa, shetani].***

- Waeleze wanafunzi wanyooshe mkono wanapoona neno wanalolitambua katika kadi utakayoonesha (au onesha maneno hayo ubaoni)
- Waambie kuwa utaonesha kila kadi (au utaonesha ubaoni) kwa haraka, hivyo waharakishe kunyoosha mkono pindi wanapoona neno wanalolitambua
- Chagua mwanafunzi aliyenyoosha mkono asome neno husika.

## Msamiati: (Dakika 4-5)

RUDIA maneno

## Ufahamu wa kusikiliza (Dakika 10):

Wasomee wanafunzi hadithi ifuatayo. ANGALIZO: Msamiati na maneno rejea yamekolezwa na yamepigiwa mstari. Yaandike maneno ubaoni. Unapofikia msamiati wakati wa Mwanafunzi aweze kusoma hadithi, tulia kwa muda na onesha msamiati huo ubaoni.

## Hadithi ya kusoma kwa sauti [Jina la hadithi]

- Andika jina la hadithi ubaoni
- Andika jina la mwandishi wa hadithi
- Andika jina la msanifu wa michoro

**Rejea ya neno la akiba:**

- Andika **[*theluji***] ubaoni.
- Wakumbushe wanafunzi kuwa neno hili limekwisha fundishwa.
- Waeleze walitumie katika sentensi kwa usahihi.